




Ni asubuhi. Hali ya hewa ni ya joto. Binti Mbuzi anakula majani. Alijifuta jasho usoni na kusema, "Ninahisi joto sana."



“Lazima nitengeneze kivuli kujuzuia na juu,” alisema. Hivyo alikata majani ya majimbi na kutengeneza kivuli.



Mchana hali ya hewa ilikuwa ni ya joto zaidi. Majani ya majimbi yalikauka kwa juakali.




Binti Mbuzi alikata majani ya mti. "Nitatumia majani mapana kujenga nyumba," alisema. Lakini joto liliongezeka. Upepo nao ulipeperusha majani kwenye matawi ya miti.



Siku moja Binti Mbuzi alifika kijijini. Aliwaona wanakijiji wakijenga nyumba. "Ngoja nitazame jinsi wanakijiji wanavyojenga nyumba." Binti Mbuzi alisema.



Aliwaangalia kwa muda mrefu. Alipata wazo. Binti Mbuzi alifikiria namna atakavyojenga nyumba yake. Alikimbia msituni. Alikata miti na majani ya mgomba.



Alichimba mashimo na kuweka nguzo. Binti Mbazi alisema, "Lazima nijengeta nyumba imara ambayo haitabomolewa na upendo."



Binti Mbuzi alitumia miti na majani ya migomba kutoka msituni kujenga nyumba imara.